

TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA



DHAMANA



- Kumtaka mshitakiwa kuripoti kituo cha polisi au mamlaka nyingine.
 - Kumzuia mshitakiwa kufika katika maeneo fulani au kuwa pamoja na watu fulani.
- Mdhamini ni mtu ambaye anaihakikishia mahakama kuwa mshitakiwa atahudhuria mahakama kila atakapohitajika kufanya hivyo. Hivyo, mdhamini hukubali jukumu la kuhakikisha uwepo wa mshitakiwa wakati shauri linaendelea.

4.0 MAKOSA YASIYO NA DHAMANA

Mtuhumiwa wa makosa yafuatayo hatakuwa na haki ya dhamana;

- Mauaji;
- Uhalini;
- Unyang'anyi wa kutumia silaha;
- Unajisi;
- Usafirishaji wa dawa ya kulevya kwa ajili ya biashara;
- Ugaidi;
- Utakatishaji fedha; na
- Usafirishaji haramu wa binadamu.

5.0 HITIMISHO

Dhamana hutolewa bure na ni haki ya kila mtuhumiwa. Hata hivyo ili mtuhumiwa apate haki hii ni lazima aweze kutimiza vigezo na kufuata masharti yaliyowekwa.

Kwa Maoni, wasiliana na Tume kupitia anuani ifuatayo :

Katibu Mtendaji,
Tume ya kurekebisha Sheria
Tanzania ,

Jengo la Taaluma Na. 1,
Barabara ya Mkalama
S.L. P 1718
DODOMA
TANZANIA

Barua pepe: lrct@lrct.go.tz
Tovuti: www.lrct.go.tz

1.0 UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Tume) ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa Sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kupitia na kutathmini utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na teknolojia. Aidha, Tume ina jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa umma.

2.0 DHAMANA

Dhamana ni hatua ambayo mtuhumiwa wa kosa la jinai huachiwa huru kwa mudaili kusubiri hatua za kufikishwa mahakamani au kama tayari amefikishwa mahakamani kusubiri kuendelea na shauri kwa siku zijazo.

Kimsingi dhamana hutolewa kwa kuzingatia kwamba Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania inaeleza kuwa mtu yeyote anayeshitakiwa kwa kosa la jinai, anachukuliwa hana hatia mpaka atakapotwa hatiani na mahakama yenye mamlaka.

3.0 AINA ZA DHAMANA

Kuna aina mbili za dhamana; dhamana ya polisi na dhamana ya mahakamani.

3.1 Dhamana ya Polisi

Dhamana ya Polisi hutolewa mshtakiwa anapokuwa chini ya ulinzi wa polisi au mamlaka yoyote ya uchunguzi kabla ya shauri kupeleka mahakamani.

Katika kutoa dhamana, masuala yafuatayo huzingatwa:

- Uwezekano wa mtuhumiwa kufika mahakamani pale atakapohitajika.
- Kumbukumbu za nyuma za uhalifu za mtuhumiwa,
- Sehemu anayoishi mtuhumiwa, familia na kazi yake.
- Ukubwa wa kosa na utendekaji wake.
- Usalama wa jamii kama mtuhumiwa atakuwa nje kwa dhamana
- Uwezekano wa mtuhumiwa kuingilia upelelezi akiwa nje kwa dhamana, kwa kuwatishia mashahidi au kuharibu ushahidi.

Mtuhumiwa anayeomba dhamana ya polisi anatakiwa afanye yafuatayo:-

- Awe tayari kufuata vigezo na masharti ya dhamana akiwa nje;
- Awe na mdhamini au wadhamini;
- Mtuhumiwa, mdhamini au wadhamini wawe tayari kuweka kiasi cha fedha kama ambacho kitachukuliwa ikiwa mtuhumiwa ataruka dhamana.

Endapo Askari Polisi akikataa kumpa mtuhumiwa dhamana, inatakiwa aandike kwa maandishi sababu ya kufanya hivyo.

Mtuhumiwa aliyeshindwa kufuata masharti ya dhamana, dhamana yake itafutwa na ataendelea kuwa chini ya uangalizi wa polisi mpaka pale shauri yake itakaposajiliwa mahakamani.

Ukiukwaji wa masharti ya dhamana ni kosa na ikiwa mtuhumiwa atatiwa hatiani kwa ukiukwaji huo atapewa adhabu ambayo haitazidi adhabu ya kosa aliloshitakiwa nalo.

3.2 Dhamana ya Mahakamani

Dhamana ya Mahakamani hutolewa wakati wa usikilizaji wa shauri la msingi unaendelea au wakati wa kusubiri rufaa kusikilizwa baada ya mtuhumiwa kutiwa hatiani na mahakama.

3.2.1 Masuala ya Kuzingatwa Wakati Mahakama Inatoa Dhamana

Katika kutoa dhamana mahakama huzingatia vigezo vifuatavyo;

- Uzito wa kosa na ukubwa wa adhabu.
- Usalama wa mshtakiwa akiwa nje kwa dhamana.
- Usalama wa muathiriwa endapo mshtakiwa atakuwa nje kwa dhamana.
- Uwezekano wa mshtakiwa kuruka dhamana.
- Usalama wa jamii kwa ujumla.
- Uraia wa mshtakiwa.
- Uwezekano wa mshtakiwa kuingilia upelelezi akiwa nje kwa dhamana.
- Muda ambao mshtakiwa amekaa rumande
- Hali ya kiafya ya mshtakiwa.
- Umri wa mshtakiwa (mtoto au mtu mzima).

3.2.2 Masharti ya dhamana

Katika utoaji wa dhamana Mahakama huainisha masharti yanayopaswa kuzingatwa. Masharti hayo ni pamoja na;

- Mtuhumiwa kusalimisha hati ya kusafiria
 - Kuweka zuio kwa mshtakiwa la kutoka nje ya eneo husika.
 - Kiasi cha fedha ambacho wadhamini wanachotakiwa kusaini kama bond mahakamani ikiwa mshtakiwa ataruka dhamana.
 - Mtuhumiwa kuwa na wadhamini
- Aidha, Mahakama inaweza kutoa masharti ya nyongeza kama vile;